twahara wa Manii

Manii: ni maji meupe, mazito, yanayotoka kwa matamanio ya nguvu kwa kasi, na yanafuatiwa na ulegevu, na yana harufu inayofanana na yai lililoharibika.

Nayo ni twahara, kwani lau yangekuwa najisi Mtume (s.a.w) angeamrisha yaoshwe.

Na inatosheleza, katika kuondoa manii, kuyaosha yakiwa majimaji, na kuyakangura yakiwa makavu, kwa hadithi ya Aishah t kuwa alisema: (Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akiosha manii kisha akitoka kwenda kuswali kwa nguo hiyo na mimi nikiona athari yamuosho katika ile nguo) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na katika riwaya ya Muslim: (Nilikuwa nikiyakangura manii kwenye nguo ya Mtume (s.a.w) kisha akiswalia) [Imepokewa na Muslim.]

https://www.al-feqh.com/sw/hukumu-za-najisi

al-feqh.com/sw